KOLOWA TECHNICAL TRAINING INSTITUTE
KOTETI

P.O Box 370 LUSHOTO TANGA TANZANIA +255747067564 027 2977003

JINA LA MWANAFUNZI: ……

ANUANI: ……..

YAH: MAFUNZO YA STASHAHADA YA FAMASIA KWA MWAKA WA MASOMO 2022/2023 KWA MUHULA WA MWEZI WA KUMI

Napenda kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya famasia katika **Taasisi ya mafunzo ya ufundi ya Kolowa Technical Training Institute** iliyopo Mkoa wa Tanga Wilaya ya Lushoto.

Napenda kukujulisha kuwa mafunzo haya yatakamilika baada ya miaka mitatu. Kuwasili chuoni nikuanzia tarehe **3/10/2022** na mwisho ni wiki moja tangu tarehe ya kufungua chuo.

Gharama ya mafunzo kwa mwaka ni **Sh.1,400,000** (**SHILINGI MILIONI MOJA LAKI NNE TU).**

Unaweza kulipa ada hii kwa awamu moja au mbili. Malipo yote ya Ada yanapaswa kufanywa kupitia akaunti ya chuo kwa namba**: 0150674824400 (CRDB)** yenye jina **KOLOWA TECHNICAL TRAINING INSTITUTE.**

1.0: UTARATIBU WA MALIPO NI KAMA IFUATAVYO:

1.1: MALIPO YA AWALI YA CHUO

Mwanafunzi anatakiwa alipe malipo ya awali kiasi cha shilingi **750,000/=** kabla hajawasili chuoni.

1.2 MALIPO YA SERIKALI

- Shilingi **18,000/=** kwa ajili ya serikali ya wanafunzi ilipwe kabla ya kuwasili chuoni.
- Shilingi **15,000/=** kwa ajili ya ada ya uhakiki ubora (NACTVET quality assurance fee) kiasi hiki kilipwe kabla ya mwanafunzi kufika chuoni kwenye akaunti ya chuo.
- Shilingi **50,400/=** kwa ajili ya malipo ya Bima ya Afya kwa mwaka kwa wasio na Bima. Fedha hii ilipwe kwenye akaunti ya chuo sambamba na ada.

1.3: MALIPO YA AWAMU YA PILI YA CHUO

Kiasi cha shilingi **750,000/=** kitalipwa mwanzoni mwa muhula wa pili.

1.4: ADA YA MITIHANI YA NACTVET

- Shilingi **150,000/=** kwa ajili ya ada ya mitihani wa NACTVET ilipwe mwanzoni mwa muhula wa pili wa masomo.

2.0: UTHIBITISHO WA AFYA YA MWANAFUNZI

Kabla ya kuripoti chuoni, hakikisha afya yako imepimwa na daktari kwenye Hospitali au kituo cha Afya kinachotambuliwa na Serikali. Mara ufikapo chuoni, utatakiwa kumkabidhi Mkuu wa chuo cheti (Medical Certificate) kutoka kwa daktari aliyekupima.

3.0: NIDHAMU NA UTII UWAPO CHUONI

Wakati wote uwapo chuoni, utatakiwa kutii sheria za Nchi na za chuo. Masuala yote ya wanafunzi chuoni yatashughulikiwa na Uongozi wa Chuo.

4.0: SARE ZA CHUO

4.1 WANAFUNZI WA KIKE

Magauni mawili (2) meupe ya mikono mifupi na urefu chini ya magoti usio pungua sentimita kumi (10cm).

Viatu vyeupe, vyeusi au kahawia vyenye visigino vifupi na soksi nyeupe.

Makoti mawili meupe ya mikono mirefu, yawe marefu chini ya magoti urefu usiopungua sentimita kumi (10cm).

4.2 WANAFUNZI WA KIUME

Suruali mbili (2) za rangi ya kaki (suruali ya kitambaa).

Mashati mawili rangi nyeupe na mikono mifupi.

Viatu vya ngozi nyeusi au kahawia.

Makoti mawili meupe ya mikono mirefu, yawe marefu chini ya magoti urefu usiopungua sentimita kumi(10cm).

Ni muhimu kuhakikisha kwamba mavazi yanatunza heshima yako na ya chuo, hivyo mavazi yasibane wala kuangaza kwa namna inayoonesha maumbile ya mwili. Wanafunzi wanatakiwa kuvaa nguo za heshima wakati wote atakapokuwa chuoni.

Hali ya hewa ya LUSHOTO niya baridi hivyo unashauriwa kununua sweta nyeupe lisilo na maandishi wala picha yoyote.

5.0 MAHITAJI YA USAJILI.

Picha nne passport size za hivi karibuni kwa ajili ya kumbukumbu.

Cheti halisi (original) cha kuhitimu kidato cha nne.

Vitabu vya ziada katika kozi husika inapowezekana.

Vifaa vya kuandikia mfano kalamu, rula, madaftari n.k

Rimu moja ya karatasi nyeupe (A4)

Shuka 4, Mto1, Blangeti1, chandarua 1 taulo na foronya.

6.0 VIFAA MUHIMU

Laptop

Scientific Calculator

10. MCHANGANUO WA MALIPO YA ADA KWA MWAKA WA MASOMO 2022/2023

NO.	ITEM	Mwaka1	Mwaka2	Mwaka3
1	Adaya Mafunzo	**1,400,000.00**	**1,400,000.00**	**1,400,000.00**
2	Kitambulisho	**10,000.00**	**-**	**-**
3	Fedha ya tahadhari	**10,000.00**	**-**	**-**
4	Gharamaza za Mitihani ya ndani	**50,000.00**	**50,000.00**	**50,000.00**
5	Usajili wa mwanafunzi kila Muhula	**15,000.00**	**15,000.00**	**15,000.00**
6	Kompyuta Na Mtandao	**15,000.00**	**15,000.00**	**15,000.00**
7	Kusimamia kazi ya Utafiti			**22,000.00**
8	Mahafali			**50,000.00**
9	Mafunzo kwa vitendo(Field)		**50,000**	
	JUMLA	**1,500,000.00**	**1,530,000.00**	**1,552,000.00**

AWAMU ZA KUFANYA MALIPO

		MWANZO WA MUHULA WA KWANZA	MWANZO WA MUHULA WA PILI
	MWAKA 1	**750,000**	**750,000**
	MWAKA 2	**765,000**	**765,000**
	MWAKA 3	**776,000**	**776,000**

11: MALAZI

Hosteli za chuo zipo za kutosha na wanafunzi wote watapaswa kuishi ndani ya chuo na gharama kwa mwaka ni **Sh**. **400,000/=** (Shilingi laki nne tu). Ili mwanafunzi aweze kupokelewa anatakiwa alipe malipo ya muhula mmoja kwanza ambayo ni **Sh. 200,000/=** (shilingi laki mbili tu). Malipo ya awamu ya pili yafanyike mara mwanafunzi anapoingia muhula wa pili wa masomo. Malipo haya yafanyike kupitia akaunti ya chuo.

12: CHAKULA

Chuo hakitoi huduma ya chakula, hata hivyo huduma hii hupatikana kwa gharama nafuu katika migahawa iliyopo mazingira ya chuo.

13: MAELEKEZO KUHUSU MAHALI CHUO KILIPO

Chuo kipo MAGAMBA katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto Mkoa wa Tanga.Ukitokea upande wa Kaskazini kama Arusha, Moshi n.k au upande wa Mashariki, Kusini na katikati ya Nchi yaani Dar es Salaam, Morogoro, Mtwara au Dodoma panda basi liendalo LUSHOTO MJINI. Usisite kutupigia simu kwa msaada zaidi.

KA RIBU SANA LUSHOTO-MAGAMBA.